**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Arobaini na Nane – Tarehe 12 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huu ni Mkutano wetu wa Kumi na Moja na hiki ni Kikao cha Arobaini na Nane, kwa mujibu wa ratiba ya kazi zetu leo ndani ya Bunge, sasa tunaweza kuanza kazi zetu rasmi na ninaomba Katibu atuongoze tunaanza na nini asubuhi ya leo, Katibu!

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Katibu. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Hati za Kuwasilishwa Mezani na Hati yetu leo inaletwa na Waziri wa Fedha, namwona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, kwa niaba ya Waziri wa Fedha.

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):-**

Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 (*Monitory Policy Statement for the Year 2013/2014).*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, kwa kuweka Hati hiyo Mezani.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na agenda inayofuata, Katibu!

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye ajenda ya maswali na swali letu la kwanza leo, linaenda Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na linaulizwa na Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhammed, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Thuwayba!

Na. 386

### Kuhusu Uchafuzi wa Mazingira Kutoka Viwandani

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED** aliuliza:-

Kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira unaotokana na shughuli za uwekezaji katika viwanda kama vile vya nguo, vitambaa vya kanga na pengine husababisha mlipuko wa maradhi kwa wananchi wanaotumia maji yanayotoka katika viwanda hivyo:-

Je, Serikali ina mpango gani kuzuia hali hii?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhammed, Mbunge (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kudhibiti na kuzuia uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda, Serikali imeandaa na kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ambayo inahimiza Tathimini ya Athari za Mazingira (*TAM*) ifanyike kabla ya kuanzishwa kwa viwanda na vile vilivyoanzishwa kabla ya Sheria hii vinapaswa

kufanyiwa Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*). Mwaka 2011/2012, jumla ya viwanda 31 vilipewa hati za ya tathimini ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Sheria hiyo inaelekeza Serikali za Mitaa kuteua au kuajiri Maafisa Mazingira ambao wataratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria hii katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kituo cha Uzalishaji Bora Viwandani (*Cleaner Production Centre of Tanzania – CPCT),* imeendesha mafunzo na kufanya tathimini kwa zaidi ya viwanda 69 hapa nchini ili kubaini maeneo na kubuni mbinu za kuongeza ufanisi katika mchakato wa uzalishaji katika viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani, imeanzisha kitengo cha Polisi wa Mazingira ndani ya Jeshi la Polisi ili kuimarisha uwezo wa Baraza katika kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea kusisitiza na kuhumiza wenye viwanda hapa nchini kutumia teknolojia bora za uzalishaji viwandani zinazozingatia hifadhi ya mazingira ili kuleta tija na kuleta maendeleo endelevu. Aidha, napenda kutoa wito kwa Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri za Majiji, Manispaa, Wilaya na Miji kuendelea kuboresha usimamizi wa Sheria na Kanuni za hifadhi ya mazingira katika maeneo yao.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Serikali imeandaa na kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ambayo inahimiza tathimini ya athari kwa mazingira na kwa kuwa kuna viwanda ambavyo bado havitekelezi sheria hiyo mpaka hivi sasa. Je, ni hatua gani mtakazo zichukua kwa wamiliki wa viwanda hivi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika swali langu

la msingi ni kwamba viwanda vyote kabla ya kuanzishwa ni lazima vifanyiwe *Environmental Impact Assessment* na vile vilivyoanzishwa kabla ya mwaka 2004 vinatakiwa vifanyiwe *Environmental Audit.* Hata hivyo, Baraza la Mazingira limeendelea kukagua viwanda hivi na pale ambapo linakuta kiwanda bado hakijatimiza masharti, basi kinapewa adhabu kulingana na sheria yenyewe. Wakati mwingine tunafikia hadi kuvifungia viwanda au mahoteli yanayohusika ili kuhakikisha kwamba sheria inafuatwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Wizara ina *program* ya kutoa elimu kuhusiana na mambo ya uchafuzi wa mazingira katika bandari zetu. Pia najua Wizara imeanzisha Kitengo cha Polisi kitakacho-*deal* na wale wote ambao wanachafua au kuharibu mazingira ikiwepo katika mikondo ya ya mito. Sasa napenda kujua mpaka sasa hivi, Kitengo hicho cha Polisi, kimeshughulikia watu wangapi ambao wanaharibu mazingira katika viwanda, bandari pamoja na mikondo ya mito?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikosi hiki kimeanzishwa mwaka jana na tayari tumeanza kufanya nacho kazi kwa pamoja. Ni watu wengi tayari wameingia katika mkondo ule. Labda nimpe tu taarifa kwamba, Kikosi hiki kina makao yake Makuu Dar es Salaam lakini kwa kutumia mtandao wa Polisi katika Mikoa, kupitia kwa *RPC* na Polisi Jamii, Kitengo hiki cha Polisi kina uwezo wa kushirikiana na *Environmental Auditors* wetu walioko katika Wilaya zetu na tutaendelea kushirikiana nacho. Niwaombe tu Watanzania wenzangu kupitia kwa viongozi wa Halmashauri pamoja na Wabunge kwamba Sheria yetu ya Mazingira inatoa maelekezo kuweza kushughulikia wachafuzi wa mazingira katika sehemu uchafu unapofanyika. Kuna *Environmental Officers* katika Kata, Wilaya na Mitaa yetu, tuwatumie hawa ili waweze kushirikiana na Kikosi hiki ili kuhakikisha kwamba wachafuzi wa Mazingira wanachukuliwa hatua zinazostahili.

**MHE. KAPT. KOMBA D. KOMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wasiwasi wa uchafuzi wa mazingira katika Ziwa Nyasa na kupelekea samaki kuelea na kuja nchi kavu wakiwa wamekufa na watu wanawaokota samaki hao wanakula. Je, Serikali ipo tayari kupeleka wataalam kule na kuchunguza ni kitu gani hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, imetoa mamlaka katika ngazi mbalimbali za Serikali ikiwepo Halmashauri kuteua Wasimamizi wa Mazingira. Kwa hiyo, Afisa anayehusika na mazingira Wilaya ya Nyasa, huyo ni lazima ahakikishe kwamba Ziwa hilo liko kwenye usalama. Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe kwenye Halmashauri hiyo, kwa hiyo, nikuombe uwasiliane na msimamizi wa mazingira katika eneo lako ili mhakikishe kwamba Ziwa hilo liko katika hali ya usalama.

Na. 387

**Kulinda Vyanzo vya Maji ili kuzuia Ukame**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Mabadiliko ya tabia nchi yameathiri mazingira ya nchi kwa kiasi kikubwa ikiwemo ukame katika maeneo mbalimbali:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji nchini ili kuepusha ukame?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhesmimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudencia Kikwembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe kuwa mabadiliko

ya hali ya tabia nchi yameathiri mazingira ya nchi kwa kiasi kikubwa ikiwemo ukame katika maeneo mbalimbali. Ili kudhibiti athari hii, Serikali imeandaa Sera, Sheria na Mikakati mbalimbali. Mwaka 1997 Serikali iliandaa Sera ya Taifa ya Mazingira ambayo pamoja na mambo mengine ililenga katika kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji na hewa. Aidha, mwaka 2004, Serikali ilitunga Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20, ili kuhakikisha kila Mtanzania anaishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya na kuweka muundo wa kisheria na kitaasisi katika usimamizi wa mazingira na kufafanua majukumu na uwajibikaji katika ngazi zote kuanzia ngazi ya kitongoji hadi ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006, Serikali ilipitisha Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Aidha, mwaka 2008 Serikali ilipitisha Mkakati wa hatua za haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Mwaka 2012 Serikali iliandaa Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*National Climate Change Strategy*) ili kuwezesha wananchi kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi na kushiriki katika juhudi za kupunguza athari hizo ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti na hifadhi ya vyanzo vya maji. Mkakati huu ulizinduliwa rasmi tarehe 21 Machi, 2013 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Waheshimiwa Madiwani pamoja na uongozi wa Wilaya katika ngazi zote kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati iliyopo kwa faida yetu na ya vizazi vijavyo.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri hayatofautiani sana na Swali Na.386, napenda tu niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali mwaka 2008 ilipitisha mkakati wa hatua za haraka wa kuhifadhi mazingira ya bahari, ukanda wa pwani, maziwa mito na mabwawa, je, ni hatua zipi za vitendo ambazo zimechukuliwa ndani ya mikakati hiyo iliyopitishwa mwaka 2008 kuhakikisha maziwa, mito na mazingira ya bahari hayaharibiwi na hayapotei kwa mfano Ziwa Rukwa ambalo liko hatarini kupotea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo ni za kuonekana zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuhakikisha kwamba wafugaji ambao siyo endelevu wanaondolewa katika mabonde. Kwa mfano, Bonde letu la Ihefu, wafugaji zaidi ya laki tatu waliondolewa na wafugaji waliovamia katika mabonde yetu kule Mkoani Kagera kutoka nchi za nje nao wameondolewa na wale waliopo wanaendelea kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mikoa pamoja na Wilaya ilielekezwa kuainisha vyanzo vyote vya maji ili waweze kuvitunza. Napenda tena nitoe rai kwa wananchi wote pamoja na Wabunge kwamba ni wajibu wa Halmashauri zetu kutambua vyanzo vyote vya maji. Tutafahamu kwamba shughuli za maendeleo zinafanyika katika sehemu ambako binadamu wanaishi. Hivyo ni Wilaya, ni Kata, Kitongoji na Mtaa vinavyofahamu kwamba chanzo cha mto huu au maji haya kiko sehemu gani. Niwaombe tena kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tuendelee kushirikiana ili kuhakikisha kwamba tunalinda vyanzo vyetu na tunahakikisha kwamba hatuna uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo yetu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro unanyemelewa na ukame na karibu mito yote ambayo inatiririka kutoka Mlima Kilimanjaro inakauka. Jambo hili

linahatarisha theluji juu ya mlima Kilimanjaro nayo kuyeyuka. Je, ni mpango gani madhubuti ambao Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii inao ili kuhakikisha kwamba mlima unaendelea kuhifadhiwa na mazingira ya ule Mkoa yanalindwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewe tu kwamba kinachosababisha theluji kupungua juu ya Mlima Kilimanjaro ni uharibifu wa mazingira ambao umefanya mvua na baridi kupungua katika maeneo hayo. Hivyo, ni wajibu wa kila mmoja wetu kuanzia Ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa na Wilaya zinazozunguka mlima huo, kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Mkoa wa Kilimanjaro umepiga marufuku kabisa ukataji wa miti na naomba niwaombe wandelee na msimamo huo. Vilevile wana *project* ambayo inajaribu kurudisha uoto wa asili katika maeneo yanayozunguka Mlima Kilimanjaro. Tutashirikiana pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanalindwa na uoto wa asili unabaki.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Zile mita 15 ambazo zimewekwa na Serikali kwa ajili ya kuhifadhi maji ni kidogo sana na hivyo kusababisha maji kuendelea kuisha. Je, Serikali inaonaje sasa kuongeza kiwango cha upana wa eneo ili hifadhi ya maji iweze kuwepo pale?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante lakini bado sijamwelewa, ni eneo gani analozungumzia?

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE**: Vyanzo vya mito!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mito ni mita 30 siyo 15

na ufukwe wa bahari ni mita 60. Kwa hiyo, hii sheria inazungumza hivyo. Labda niseme tu kwamba, mabadiliko ya tabia nchi ni janga la kimataifa. Kwa Waafrika, tunaweza kulikabili janga hilo kama tutaweza kulinda vyanzo vyetu vya maji vizuri, kwa sababu vyanzo vya maji vina uoto wa asili na una asili ya kunyonya gesijoto hizo ambazo ni *carbon dioxide* pamoja na fukwe lakini vievile tukipanda miti ya kutosha, tuna uwezo wa kunyonya hizo gesijoto na kupunguza athari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu uzoefu unaonyesha kwamba nchi ambazo zinazalisha sana gesijoto ndizo zinazopata athari kubwa. Kwa hiyo, hata sisi hapa Tanzania, Mikoa ambayo haizingatii taratibu za kuhifadhi mazingira ndiyo itakayopata zaidi athari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa ufupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAZINGIRA):** Kwa hiyo, nitoe wito kwamba watu wote pamoja na sisi Wabunge tushirikiane kupanda miti ya kutosha na kuhifadhi vyanzo vya mito pamoja na ardhi oevu na chepechepe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru, Waheshimiwa Mawaziri naomba majibu yenu yawe mafupi, kipindi cha maswali tunapenda maswali mafupi na majibu mafupi lakini yenye kujenga hoja. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 388

**Uendelezaji Michezo kama Ajira**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI (K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR)** aliuliza:-

Michezo ni ajira kubwa sana duniani kwa sasa katika michezo ya aina mbalimbali kama vile mpira wa miguu, pete, wavu, ridhaa na kadhalika:-

(a) Je, kwa nini Serikali inapendelea mchezo wa

aina moja tu (mpira wa miguu) kwa kutafutia udhamini mkubwa tofauti na michezo mingine?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutafuta wafadhili wa michezo hiyo mingine ili vijana wenye vipaji vya michezo hiyo waweze kuinuliwa?

(c) Timu ya Taifa (*Taifa Stars)* kila siku inazidi kushuka viwango vya *FIFA*, je, ni tatizo lipi linalosababisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein N. Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina upendeleo katika aina yoyote ya michezo. Ni kwa sababu hiyo Serikali ilishawahi kuajiri Makocha kutoka nje ya Tanzania kwa ajiri ya michezo ya riadha, ngumi, netiboli, judo na mpira wa miguu. Aidha, udhamini katika sekta ya michezo huzingatia namna chama au shirikisho la michezo husika lilivyojiandaa na kuweza kushawishi wafadhili.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa mstari wa mbele na itaendelea kuhakikisha vyama na mashirikisho ya michezo yanakuwa na miundo, uongozi thabiti na mikakati endelevu ili hatimaye kuwavutia wafadhili katika uendeshaji wa michezo husika.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, kigezo kikuu cha viwango vya *FIFA* ni michezo kati ya timu ya Taifa na timu za mataifa mengine. Hata hivyo, kwa takwimu za sasa za *FIFA*, Tanzania imekuwa ikipanda katika viwango vya *FIFA* tofauti na ilivyokuwa miaka 10 iliyopita.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Hapo awali, Tanzania ilikuwa imepata sifa kubwa sana hasa katika michezo ya riadha ambapo wanariadha mashuhuri walijitokeza na kuliletea sifa Taifa letu lakini sasa hali sivyo hivyo. Ni nini hasa ambacho kinapelekea kuanguka kwa michezo huu, ambapo tuna vijana wenye vipaji vizuri katika masuala ya riadha?

(b) Tunazo Taasisi ndani ya nchi ambazo zinajaribu kuhamasisha michezo hii ya riadha, katika Mkoa wa Simiyu kuna *Serengeti Sports Center* ambayo imeanzisha mbio za *Serengeti Marathon* na Wizara imealifiwa kuhusu hili. Je, Wizara inafanya juhudi gani kusaidia michezo hii kukua? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kweli tunakiri kwamba hapo nyuma Tanzania ilikuwa inasifika sana kwa michezo ya riadha na tulifanya vizuri lakini hapa katikati tumekuwa hatufanyi vizuri. Nataka niwahakikishie tu kwamba Serikali imeendelea kujipanga na chama hiki cha riadha sasa kimepata uongozi mpya na umekuja na mikakati ambayo tayari Wizara inawasiliana nao kuona kwamba tunaibua vipaji kuanzia shule za misingi hatimaye tuendelee kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Dokta Kamani na alinishirikisha katika michezo ambayo ameiandaa kule Simiyu na sisi kama Wizara tutaendelea kumpa mshikamano na tayari tunaandaa baadhi ya ushauri ambao unaweza ukafanikisha tukashirikiana na Wizara zingine ili kuona kwamba mashindano ambayo Dokta Kamani na Taasisi wanayoshirikiana nayo, yanaenda vizuri katika Mkoa wa Simiyu.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tanzania sasa hivi pale Dar es Salaam tuna uwanja

mzuri wa kandanda. Je, Waziri atatuambia ni lini wataweka namba kwenye viti ili na sisi tuingie kwa utaratibu unaokubalika duniani?

**MWENYEKITI**: Ahsante kwa swali fupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na usumbufu na hata kuathiri mapato kutokana na kwamba uwanja ule bado hakujawa na viti, lakini sisi tumelipokea na tuko katika hatua za mwisho za kuhakikisha hata tiketi zenyewe sasa zinakwenda kwa njia ya kisasa zaidi na kunakuwa na vizuizi ili kudhibiti mapato na hilo la viti tutalishughulikia.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Timu za Simba na Yanga zinatakiwa kushiriki Kombe la Kagame Sudan, Darfur, lakini hali ya usalama kule ni tatizo. Je, nini tamko la Serikali kuhusu usalama wa timu zetu hizo mbili *in case* kama zikienda Sudan? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na taarifa za kutokuwa na hali ya usalama huko Darfur, Sudan na nimshukuru sana Waziri wa Mambo ya Nje alilitolea Kauli suala hili na sisi ndani ya Serikali tunazo taarifa za kutosha kwamba Sudan hakuna usalama na nchi zingine zimeendelea kujitoa. Msimamo wa Serikali ni kwamba hatuwezi kupeleka timu mahali ambapo hapana usalama. *(Makofi)*

Na. 389

**Ahadi ya Kuboresha Usikivu wa Radio ya Taifa *(TBC Taifa)* Nchini Kote**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Serikali iliahidi ndani ya Bunge juu ya koboresha usikivu wa Radio ya Taifa (*TBC* Taifa) nchini kote lakini bado redio hiyo husikika kwa tabu kwenye maeneo mengi nchini ikiwemo Tandahimba:-

Je, lini mpango huo utakamilika rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMDUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iliahidi ndani ya Bunge lako Tukufu juu ya kuboresha usikivu wa *Radio* ya Taifa (*TBC* Taifa) nchini kote. Aidha, Serikali inatambua tatizo la usikivu wa *Radio* kwa baadhi ya maeneo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha matangazo ya *TBC* yanamfikia kila Mtanzania popote alipo nchini. Katika kutekeleza ahadi hii, Serikali inaendelea na mpango wake wa kufunga mitambo ya *Radio* katika Miji Mikuu ya Mikoa yote nchini kwa kadri fedha zinavyopatikana na baada ya hapo katika Miji yote ya Wilaya. Hadi sasa, matangazo ya *Radio* ya *TBC Taifa* yanasikika katika Mikoa 21 na Wilaya kadhaa ikiwemo Wilaya ya Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tandahimba inapata matangazo kwa kiwango cha kuridhisha kupitia kituo cha kurushia matangazo kilichoko Newala katika masafa ya *FM* ya 100.9 *MHz TBC* Taifa na 97.4 *MHz* kwa *TBC FM*. Aidha, kwa baadhi ya maeneo ya tambarare yasiyo na vizuizi vya milima, Wilaya ya Tandahimba hupata pia matangazo ya *TBC* kupitia kituo cha *FM* cha Lindi katika masafa ya 107.1*MHz TBC Taifa* na 93.5MHz *TBC FM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha *Radio* ya Taifa *(TBC Taifa)* inasikika nchini kote.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, mimi naomba nimwambie Mheshimiwa

Naibu Waziri, nimesikitishwa sana na majibu yake. Mimi natoka Tandahimba, mimi ndiye ninayeijua Tandahimba. Wilaya ya Tandahimba maeneo mengi yanapata matangazo ya *TBC* usiku tena kwa shida sana na sasa wananchi wameamua kusikiliza Radio Nangare ya Musumbiji na kidogo hivi karibuni tu Radio Newala ambayo imeanza kazi miezi mitatu iliyopita, tena kuna muziki tu kwa sababu wako kwenye majaribio. Hivi kwa kusikika *TBC* usiku tu huko ni kupata matangazo ya kuridhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata habari ni haki ya Kikatiba lakini Watanzania wengi hasa wanaoishi vijijini wamekuwa wakipata shida ya kupata matangazo kwa kupitia vyanzo vingine kama *Television*, hapa *Radio* ndiyo sanasana inayowasaidia...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Njwayo, swali.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Kwa sababu *TBC* ni Shirika linalomilikiwa na Serikali kwa kiwango kikubwa, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwekeza kwa kiwango kikubwa na haraka sana tukamaliza kadhia hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMDUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mimi nilidhani kwamba haisikiki kabisa, kumbe inasikika usiku. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba marekebisho hayo tumesema kwamba kuna wakati mwingine kunakuwa na matatizo, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba katika bajeti yetu tuliyowasilisha hapa, tumeeleza mpango wa *TBC* na tukaongeza na fedha, lengo letu ni kuhakikisha kwamba matangazo yanafika kote nchini. Kwa hiyo, tupeni muda na fedha mlizozipitisha tuna mipango ya kujenga mitambo ya kisasa kwa kila Mkoa ili kuona kwamba matangazo yanafika nchini kote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika kuwekeza katika suala zima hili, ni kwamba Serikali imetenga shilingi bilioni tisa, tupeni nafasi, tuone kwamba tunazitumiaje fedha hizo ili matangazo yaweze kupatikana nchini kote.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilikuwa naomba tu nimuulize Naibu Waziri kwamba, sambamba na usikivu wa *Radio* kwenye maeneo ya pembezoni, lakini bado kuna vyombo vingine vya habari ambavyo vimetishia kujitoa kwenye king'amuzi na *Star TV* wameshajitoa, je, nini hatma ya tetesi hizo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na mimi nimesoma kwenye magazeti namna ambavyo kuna mvutano kati ya *Star Times* na *Star TV* na ambavyo *TCRA* imeweza kulishughulika suala hili. Naomba wanipe nafasi ili Wizara yangu na Wizara ya Mawasiliano tufanye kazi hiyo ya kuona kwamba tunatatua tatizo hili.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali langu ni dogo tu. Kwa kuwa sasa hivi tunaendelea na mchakato wa Katiba na tayari *TBC* haisikiki Tanzania yote, je, ni nini hatua za dharura ambazo Serikali itaweza kuzifanya ili *TBC* isikike kila pahali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mpango wa Serikali na fedha zilivyotengwa lakini pia Tume ya Katiba yenyewe imejipanga namna itakavyotoa vipindi katika redio na sisi kama Serikali tunaona umuhimu wa wananchi kupata habari zinazohusiana na Katiba, Serikali imejipanga na Tume ya Katiba pia kuhakikisha kwamba wananchi wanapata fursa hiyo.

Na. 390

**Askari wa Jeshi la Polisi Wanaohamishwa Vituo vya Kazi**

**MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MHE. MESHACK J. OPULUKWA)** aliuliza:-

Je, Serikali inasema nini juu ya Askari wa Jeshi la Polisi kote nchini ambao wamehamishwa vituo vya kazi bila

kulipwa stahili zao kama wale waliohamishwa toka Wilaya ya Meatu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu ya kazi za Jeshi la Polisi Askari wamekuwa wakihamishwa ili kukidhi mahitaji ya utendaji kazi. Kwa mwaka wa fedha 2009 hadi mwezi Mei, 2013, madeni ya Askari Polisi yanayohusisha stahili mbalimbali yalikuwa Tshs.28,051,997,125.01. Kati ya madeni hayo Tshs.11, 688,529,141.01 yamehakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani *(Internal Auditor General*) na madeni yaliyobaki ya jumla Tshs. 16,363,467,984.00 hayajahakikiwa. Zoezi la uhakiki wa madeni hayo linaendelea na pindi litakapokamilika na fedha kutolewa na Hazina, madeni hayo yakiwemo ya Askari wa Meatu aliowataja Mheshimiwa Mbunhge yataanza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nichukue nafazi hii kuwashukuru Askari wote wanaodai stahili zao mbalimbali kwa utulivu na uvumilivu wao wakati wa Serikali ikitafuta ufumbuzi wa tatizo hili.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, amewapongeza Askari kwa kuwa na subira bila kupata stahiki zao. Ningeomba sasa Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge lako Tukufu leo, ni lini sasa hawa Askari wetu watapewa stahiki zao ili waendelee na maisha kama Askari wa kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ucheleweshwaji wa stahiki za Maaskari nchini kwetu umepelekea Askari wetu kuvaa sare duni, ambazo zimejaa viraka kila sehemu...

**MWENYEKITI:** Swali, swali.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Ninaomba Mheshimiwa Waziri atuambie, anatoa kauli gani kuhusu hali hii ya kuwadhalilisha Askari wetu hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema katika majibu yangu ya msingi kwamba, tayari madeni haya yanahakikiwa na Mkaguzi wa Ndani na yatakapokamilika, Hazina watalipa fedha. Tayari Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wameshawaandikia Hazina barua juu ya madeni ambayo tayari yamehakikiwa na mengine ambayo bado wafanye haraka ili watu hawa waweze kupata haki zao walipwe haraka iwezekanavyo. Ni nia ya Serikali kuona kwamba wanalipwa mapema kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba Serikali haijawa na nia yoyote ya kuwadhalilisha Askari wake na kwamba suala hili linazingatiwa katika bajeti na kuona kwamba Askari wetu wanakuwa nadhifu na wanatenda kazi zao vizuri.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Askari ambao wamekuwa wanahamishwa Mkoa wa Kigoma, wamekuwa hawahamishwi nje ya Mkoa, wanatolewa Kasulu wanapelekwa Kibondo, wanatolewa Kibondo wanapelekwa Manyovu, jambo ambalo linasababisha uhalifu kuwa mkubwa kwa sababu watu hao wanazoeana na wananchi. Mfano, wiki iliyopita kwenye Wilaya ya Kibondo yametekwa magari saba na matukio zaidi ya sita ya ujambazi yamefanyika, watu wanapigwa risasi, kwa nini Serikali inawahamishia Maaskari humohumo kwenye Mkoa kuliko kuwapeleka Mikoa mingine na haiwalipi fedha hizo?

**MWENYEKITI**: Utajibu swali moja tu la msingi, hatujibu (a) na (b).

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la uhamisho wa Askari yawezekana ni kuongeza ufanisi, kuongeza nguvu mahali fulani, ni ili Askari waweze kutekeleza majukumu yao vizuri zaidi. Suala nani aende wapi, ni suala la kiutendaji na linaamuliwa na utawala uliopo. Kwa hiyo, nataka niseme tu si nia ya Serikali kuwazungusha Askari hao hapohapo, inawezekana kwamba ufanisi wao upo katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nataka niseme Askari wataendelea kuhamishwa kwa sababu hizo nilizozitaja kwamba ni ili kuongeza nguvu na ufanisi na madeni yao yatakapohakikiwa watalipwa fedha zao zote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtutura!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Dhamira yangu ilikuwa ni swali Na. 391na siyo hili, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Naomba tuendelee.

Na. 391

**Kukarabati Majengo Makongwe ya Askari Polisi**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Serikali inajitahidi kuwajengea Askari nyumba bora zinazoendana na mila na desturi za Mtanzania:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu kufanyia ukarabati majengo makongwe ya Askari Polisi yaliyopo kwenye hali mbaya?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba majengo mengi yanayotumiwa na Askari Polisi hapa nchini ni chakavu na ambayo hayakidhi mahitaji halisi ya maisha ya sasa. Aidha, Serikali inatambua ukongwe wa baadhi ya majengo anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuyafanyia ukarabati majengo yote yenye hali mbaya na kuendelea kujenga majengo mapya kwa ajili ya makazi ya Askari. Hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kuboresha makazi ya Askari kupitia bajeti, mpango wa maboresho na hata ushirikiano wa wadau mbalimbali zikiwemo nchi rafiki. Serikali itaendelea kufanya ukarabati wa majengo ya makazi ya Askari yaliyo katika hali mbaya kutokana na bajeti ya Serikali na ubunifu mwingine.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uzoefu mkubwa wa kupewa ahadi za kila siku humu ndani. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa mara nyingi wakipewa ahadi kama za mtoto wa kuku akimdai mama yake kunyonya, mama yake humwambia, 'lala kipanga anakuja, lala kipanga anakuja', ndiyo hiki Mheshimiwa Waziri anachoniambia leo. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Riziki alikuwa akiimba ahadi ya kuku kwa mwanaye)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Waziri wa Mambo ya Ndani aliyekuwepo alifanya ziara nadhani nchi nzima na aliona hali halisi ilivyokuwa mbaya ya majengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alithibitishie Bunge hili na wananchi wa Tanzania pamoja na Askari Polisi ni lini watajengewa majengo yale ili wasiendelee kulala ndani ya majengo mabovu wakadhalilika Askari wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa kuna mfuko wa fedha za maendeleo, naomba basi Serikali au naishauri itenge angalau 25% kila mwaka kuanzia bajeti ya mwaka huu ili waweze kukarabati majengo yale ili tusiendelee kuyapoteza na yakaporomoka kabisa kuwa kufikiria yale mapya tu ambayo tumeyajenga? Je, Waziri anakubaliana na ushauri huo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme tu kwamba si ahadi hewa. Serikali katika hili inakusudia kufanya hivyo ambavyo tumejibu hapa. Nataka nimhakikishie tu kwamba Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani alikuwa katika Mikoa ya Pemba, amefanya ziara amepita Micheweni, Chakechake, *Line Police,* Kengeja na kadhalika, tumeona namna ambavyo majengo haya yamechakaa. Nataka nimhakikishie kwamba Serikali inakusudia kuboresha makazi haya. Ushauri wake alioutoa tumeupokea na tutaufanyia kazi.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Hali ambayo inazungumzwa juu ya majengo ya Polisi kwa Wilaya yetu ya Tunduru ni ya kusikitisha sana hasa ukizingatia kwamba Tunduru ni eneo kubwa na vilevile ni Wilaya ambayo ipo mpakani, wajibu wa Polisi ni mkubwa sana na hasa ukizingatia kwamba wahalifu wa kutoka nje ya nchi yetu na wa ndani ya nchi yetu huwa wanakimbilia Msumbiji. Kwa hiyo, Polisi wanachoka na wakirudi nyumbani wanakuta majengo na malazi ni hafifu sana. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja kabisa ya kutoa upendeleo wa aina yake kwa Wilaya ya Tunduru ili Polisi wale wapate makazi mazuri ambayo yatawafanya waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye na mimi nilikuwa Jimboni kwake, niliwahi kufanya kampeni kwake na nimekaa na *RAC* naelewa maeneo yale ya mpakani na namna ambavyo Askari hao wanavyofanya kazi hizo na ninafahamu jengo hilo na makazi hayo. Niwaahidi Wabunge wote kama ambavyo nyumba za Askari pale *Kilwa Road* zilivyokuwa chakavu mpaka sasa Serikali imefanya jitihada hizo ambazo mnaziona, upo mpango wa maboresho kwa nchi nzima ili kuona kwamba Askari wetu wanapata makazi mazuri na ofisi nzuri kwa nchi nzima.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ni kipindi kirefu sana baadhi ya Askari wamekuwa wanakarabati nyumba zao kwa kutumia gharama zao wenyewe. Je, Serikali inasema nini kuhusu Askari hawa kurudishiwa gharama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba tumepokea malalamiko hayo ambayo anayasema Mheshimiwa Mbunge, naomba tukae naye tuone kwamba tunalishughulikiaje suala hili.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na swali linalofuata, bado tuna maswali mengi na litaulizwa na ...

*(Hapa Mheshimiwa Aeshi Aliingia Ukumbini baada ya kuwa nje kutokana na kesi ya uchaguzi iliyokuwa ikimkabili huku baadhi ya Wabunge wakipiga Makofi na Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Kuna nini tena huko?

Mheshimiwa Aeshi naomba uketi, naomba uchukue nafasi yako uketi kwa mujibu wa taratibu, naomba uchukue nafasi yako uketi.

**MBUNGE FULANI:** Hana Kiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aeshi naomba uketi! *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, *order, order, order.* Naomba utulivu, mwacheni Mheshimiwa Aeshi achukue kiti chake tuendelee na shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu.

Na. 392

**Ucheleweshaji wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa iliyoteuliwa kuwa mfano wa Kilimo Kwanza.

(a) Je, kwa nini pembejeo zimechelewa kufika katika Jimbo la Manyovu?

(b) Je, Serikali haina wataalamu wa mipango hadi kusababisha ucheleweshaji wa pembejeo nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejeo nchini unahusisha pembejeo zinazopata ruzuku ya Serikali katika bei na pembejeo zinazouzwa na wafanyabiashara kwa utaratibu wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo yenye ruzuku inaagizwa na kusambazwa kwa utaratibu maalum na makampuni na mawakala walioteuliwa ili kuhakikisha kwamba wakulima husika wanapata pembejeo hiyo kwa bei iliyopangwa na Serikali na kwamba wanapata unafuu wa bei kupitia ruzuku. Ucheleweshaji wa pembejeo yenye ruzuku umekuwa unasababisha upatikanaji wa fedha za kuchapisha vocha ambapo Wizara imelazimika kusubiri bajeti ya Serikali ipitishwe ndiyo taratibu za manunuzi zianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pembejeo ya soko huria, wafanyabiashara wa pembejeo wamekuwa wanasita kupeleka pembejeo vijijini wakati wa kiangazi kwa kuhofia gharama za uhifadhi kwa muda mrefu kutokana na wakulima wengi kusubiri mpaka mvua inyeshe ndiyo waanze kununue pembejeo. Aidha, sababu nyingine ya kuchelewa kwa mbolea yenye ruzuku, ni urasimu na ubadhirifu katika usambazaji wa vocha za pembejeo uliosababishwa na baadhi ya watendaji na mawakala wasio waaminifu ambao wamekuwa wanasababisha wizi na upotevu wa fedha na wakati mwingine pembejeo hiyo iliyokusudiwa kutokumfikia mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia changamoto zilizojitokeza, Serikali imebuni mfumo mpya wa usambazaji wa pembejeo utakaotumika katika msimu unaokuja wa 2013/2014 ambapo katika baadhi ya maeneo wakulima kupitia vikundi na vyama vya ushirika watapata mikopo ya muda mfupi yenye riba nafuu kwa ajili ya kununulia pembejeo. Mfumo huo umejadiliwa katika semina za usambazaji wa pembejeo iliyofanyika Dodoma tarehe 28 na 29 Mei na kuonekana kuwa unaweza kuleta manufaa yanayotarajiwa pamoja na kuwa utajenga uwezo endelevu wa wakulima kununua mbolea.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nipongeze juhudi za Serikali na Wizara kusaidia wakulima wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa katika majibu ya swali la msingi, Naibu Waziri amekiri kwamba fedha za kuchapisha vocha ndiyo changamoto. Je, analihakikishia Bunge hili kwamba changamoto hiyo ya fedha za kuchapisha vocha hasa kwenye vikundi vitakavyonunua na vyama vya ushirika limetatuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, je, ni lini wakuu wa Wizara hii watatembelea Jimbo la Manyovu ili watoe elimu ambayo itasababisha pembejeo isichelewe kwenye eneo langu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekiri kwamba pesa za kuchapisha vocha zimekuwa ni changamoto na hilo tumelisema kwa sababu katika utaratibu wa mzunguko wa bajeti wa miaka iliyopita, tumekuwa tunapata idhini ya kuanza matumizi ya fedha mwezi wa tisa, lakini msimu wa kupandia unaanza kwenye mwezi wa saba na nane katika baadhi ya maeneo nchini.

Kwa hiyo, kwa utaratibu huu mpya ambao sasa Bunge letu limeamua kuanza nao kwa mwaka huu, tunatarajia kwamba ifikapo tarehe 1 Julai tutakuwa na pesa tayari kupitia Wizara ya Fedha na Hazina tumekubaliana nao kwamba pesa maalum za pembejeo zile ziwe *ring fenced* na zitolewe mapema ili masuala ya vocha na pembejeo na mambo mengine yote yaweze kuwafikia wakulima kwa wakati. Kwa hiyo, naamini kwamba tatizo hili tutalipatia ufumbuzi mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la Wakuu wa Wizara kwenda kutembelea maeneo yake, Waziri wa Kilimo Eng. Chiza ameshatoa maagizo, tutasambaa wote, sisi wakuu wa Wizara yote kwenda kwenye maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba ile pembejeo inayofika siyo tunapewa hadithi ila sisi wenyewe tujionee imefika kwa wakati na wakulima wanaelimishwa matumizi sahihi ya pembejeo kwa wakati huo.

**MWENYEKITI:** Swali fupi Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kumekuwa na ucheleweshaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima karibu misimu yote lakini amelieleza Bunge na Watanzania kwamba Serikali mwaka huu imejipanga vizuri kwamba jambo hilo halitokei tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mheshimiwa Waziri awahakikishie Watanzania kwamba tumebadilisha mfumo wa mbolea na awahakikishie kwamba hiyo wanayosema mikopo kupitia kwenye *SACCOS* itafika kwa wakati na ikiwezekana awaeleze Watanzania wamejipanga kiasi gani maana msimu wa kilimo ndiyo huo unaanza sasa kwa mwaka 2013. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ruzuku umeanza mwaka 2007 na umekuwa unagubikwa na matatizo ama ya vocha ama mawakala na kadhalika. Mwaka huu tulichofanya ni kwamba tutakuwa na mifumo miwili, kwa bajeti hiyo ambayo tutapitisha nadhani kesho au wiki ijayo, tunatarajia kwamba kwenye Mfumo wa Pembejeo tutakuwa na pesa ambazozitatumika kwenye vocha na pesa ambazo zitatumika kwa utaratibu huu wa mkopo ambao Vyama vya Msingi na vyama vya uzalishaji vitakuwa vinakwenda kwenye benki, vinakopa kwa kudhaminiwa na Serikali na Serikali yenyewe ndiyo itadhamini riba ili ipungue kidogo wapate unafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema kwamba katika utaratibu huu tunaamini kabisa benki zitakazokopesha na taasisi za fedha zitanufaika katika kukopesha mapema maana ukimkopesha mtu umechelewa akija kuzalisha chini ya kiwango atashindwa kukurudishia kwa wakati. Kwa hiyo, tunafanya kazi sisi, taasisi za fedha

wakiongozwa na Benki Kuu ili kuhakikisha kwamba mfumo huu kwa upande wa mikopo unakwenda vizuri lakini pia kwa upande wa vocha nao utakuwa unapata usimamizi wa karibu.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mbolea kwa utaratibu huu wa sasa limejitokeza kwa kiasi kikubwa sana mwaka jana. Mwaka jana utaratibu mzima ulichelewa na mbolea ya kupandia imefika Kigoma kipindi ambacho watu wanakaribia kuvuna. Tukaagiza kwenye Halmashauri kwa maana ya Kikao cha Mfuko wa Pembejeo kwamba vocha zote zikusanywe ili kusudi wale mawakala wasiendelee kuwatapeli watu kwa kuwasainisha wanawapa pesa na baadaye waweze kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ningependa kujua Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba vocha zote zimekusanywa ili kusudi utapeli wa aina hiyo usiendelee kufanyika kwa sababu mpaka sasa kuna kesi kwenye kijiji cha Kaseke ambapo Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya nimewataarifu lakini hatua haijachukuliwa, Mawakala wanasambaza vocha zile wanawasainisha watu kwa shilingi 5,000/=. Naomba kujua Serikali inatoa tamko gani kuhusu vocha ambazo bado zipo uraiani? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kabisa kwamba mbolea inachelewa, mbolea wakati mwingine inafika kwa wakati, kinachotokea ni huo ubadhirifu anaouzungumza yaani hao wajanja ambao wanacheza na vocha. Mbolea inaweza kuwa ipo lakini vocha zenyewe wale wakawa wanafanya ujanjaujanja. Kwa hiyo, hilo ndiyo jambo ambalo lipo. Inawezekana mbolea pia ikachelewa lakini kubwa zaidi ni wale wanaocheza na vocha hata kama mbolea imekwishafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi ni hili la kwamba tunachukua hatua gani dhidi ya watu hawa mimi nimekwishaagiza wote wale ambao wamecheza na vocha, kwanza vocha zile ambazo hazikuhusika katika utaratibu huu,

zimezuiliwa na zimechukuliwa na Wizara kwa ajili ya kuhakikiwa kabla hazijatumika katika msimu unaofuata lakini wote walioshiriki pia tunaendelea kuchukua hatua na watafikishwa Mahakamani. *(Makofi)*

Na. 393

**Ghala la Chakula Musoma**

**MHE. VINCENT J. NYERERE:-**

Ukarabati wa ghala la chakula katika Mji wa Musoma maeneo ya Baruti Nayakato umekamilika:-

Je, ni lini ghala hilo litaanza kutumika kuhifadhi chakula ili kupunguza umbali uliopo katika kufuata chakula Shinyanga na maeneo mengine yaliyoko mbali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa ghala la kuhifadhi chakula lililopo Baruti Nyakato umekamilika kwa hatua ya awali na ghala litakuwa na uwezo wa kuhifadhi zaidi ya tani 4,500 za chakula. Ghala hilo litasaidia kupunguza umbali na gharama katika Mkoa wa Mara na maeneo ya karibu na Mkoa huo ya kufuata chakula katika maghala yaliyopo Shinyanga na maeneo mengine yaliyopo mbali na Mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA)* uko kwenye mchakato wa kujenga uzio kuzunguka ghala hilo ili kuimarisha ulinzi na usalama wa chakula kitakachohifadhiwa. Mchakato huo ni sehemu ni mpangokazi wa wakala uliopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ghala hilo linatarajiwa kuanza kutumika msimu huu wa ununuzi kwa maana ya mwaka 2013/2014 baada ya ujenzi wa uzio kukamilika na litatumika kuhifadhi nafaka kwa ajili ya kuhudumia Mkoa wa Mara na maeneo mengine ya jirani na Mkoa huo.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na ghala kukamilika, kumekuwapo na upigaji marufuku usio na tija kwa viongozi wa Serikali kuwazuia wakulima na wafanyabiashara wa Mkoa wa Mara kutumia mpaka wa Sirari kuingiza chakula wakati wa njaa na kuuza chakula nje wakati wa ziada. Je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo kwa viongozi wa Serikali kutopiga marufuku zisizo na tija? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuzuia chakula kwenda nje ya Tanzania ulikuwa umefutwa na tumeruhusu wakulima kama Sumbawanga, Songea na kadhalika kuweza kuuza chakula nje lakini jambo hilo lazima lifanywe kwa utaratibu, hauwezi kufanywa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbali ya hiyo, hata chakula tunachoingiza ndani kama kinatoka Kenya au Zambia kwa sasa hivi tuna chakula kinatoka Malawi kupitia mipaka ya Ileje, tuna chakula kinatoka Msumbiji kupitia Ruvuma na kadhalika lakini ni lazima kidhibitiwe ili chakula kile kiingie katika utaratibu unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hapa ugomvi siyo chakula kinachoingia au kutoka, ugomvi ni kufuata utaratibu. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba kwa sababu tumesikiasikia malalamiko haya ya Sirari, hatuyapati maeneo mengine lakini kwa Sirari tutatengeneza utaratibu ili tujue hasa ni kitu gani.

Pia tunakuomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wa Tarime na maeneo ya karibu muwahimize watu kufuata utaratibu katika biashara hizi ili biashara hii iende kwa amani na utulivu.

**MWENYEKITI:** Waziri majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako niongeze majibu ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sirari hasa Mkoa wa Mara, tatizo ambalo limejitokeza ni ugonjwa wa mahindi. Ugonjwa huo umeanza kuenea katika nchi na hivi karibuni nitatoa Kauli hapa Bungeni kuhusu ugonjwa huo wa mahindi. Ugonjwa huo unaenea kwa kasi ukiingiza nafaka. Kwa hiyo, ukiona wanazuia si kwamba wanazuia tu, wanachojaribu kuzuia pia ni pamoja na kuzuia ugonjwa ule usienee kwa kuingiza nafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanachotaka ni kwamba kila mahindi yanayoingia yawe yamedhibitiwa. Kwa kawaida tunapenda wakiingiza waingize unga badala ya nafaka, kwa hiyo, hilo ndiyo tatizo la Mkoa huo.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mikoa mingine iliteuliwa kuwa mfano wa Kilimo Kwanza na baadhi kutengwa kama Ghala la Taifa la Chakula, je, ni kwa nini Taifa limeendelea kuwa na uhaba mkubwa wa chakula na hasa mwaka huu ambapo Mikoa mingi haina chakula cha kutosha? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri hajakuelewa, rudia swali lako kwa ufupi, uwe *specific* kusudi aweze kuelewa.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mikoa ambayo ilitengwa kama mfano wa Kilimo Kwanza na Mkoa wa Morogoro kuitwa Ghala la Taifa la Chakula. Kama tuna Ghala la Taifa la Chakula, ni kwa nini Taifa limeendelea kuwa na uhaba mkubwa wa chakula? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuwa na Mikoa ambayo inakuwa ni Maghala ya Chakula umeanza kwa sababu katika baadhi ya Mikoa ile tuna uzalishaji mkubwa, kuanzia Ruvuma kule kwako Mheshimiwa Mwenyekiti mpaka Katavi kwa ukanda wote ule, kwa hiyo, ile Mikoa imetengwa maalum kwa ajili ya kuwa ni hifadhi ya chakula ukianzia Morogoro kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, kama uzalishaji ni mdogo, umekuwa ni mdogo tu na sababu ziko nyingi, inaweza ikawa ni ukame, matumizi mabaya au mbolea iliyoingia ilikuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya ni kwamba Mikoa ile inabaki kuwa ni hifadhi za chakula na tunataka kuweka msisitizo katika utoaji wa ruzuku na mafunzo ya kuzalisha tija kwa kiasi kikubwa zaidi ili wazalishe chakula kingi zaidi. Kwa hiyo, hili halihusiani na Mikoa hii kuwa hifadhi za chakula, ni utaratibu tu wa uzalishaji.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naamini Wizara inafanya kazi nzuri ya kujenga na kukarabati haya maghala ya chakula. Hata hivyo, kuna ghala moja ambalo hivi sasa linataka kuwa wimbo, ghala la Nkaralo Kwimba ambalo Mheshimiwa Ndassa amelipigia kelele muda mrefu na Waziri aliishaahidi kulifungua. Je, utekelezaji wake umefikia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa maghala, tuna maghala matatu katika Wilaya ya Kwimba, katika kijiji cha Manai, samahani, ghala alilolitaja Mheshimiwa Mbunge linafanyiwa ukarabati wa kulikamilisha na tunatarajia kwamba kwa mwaka huu wa fedha unaokuja 2013/2014 ghala hilo litaanza kutumika.

Hata hivyo, pamoja na kwamba lina ahadi ya muda mrefu tutafuatilia kwa karibu na tutawapatia majibu Waheshimiwa Wabunge wa Kwimba ili tupate utekelezaji wa ghala hilo.

Na. 394

**Ujenzi wa Chuo cha Kikuu cha Kilimo Mpanda**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imefanikisha kupata mdau wa kujenga chuo kikuu cha Kilimo:-

Je, ni lini Serikali kupitia Wizara ya Fedha itatoa dhamana na kuwezesha ujenzi wa chuo kikuu hicho ili angalau Ukanda wa Magharibi upate chuo kikuu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mbunge wa Mpanda wa Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilipokea maombi ya dhamana ya Serikali ya dola za Kimarekani 2.5 milioni kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, kwa ajili ya gharama za awali za ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Katavi. Maombi haya yalijadiliwa na Kamati zilizoundwa kisheria za kusimamia deni la Taifa ambazo ni: *Technical Debt Management Committee (TDMC)* na ile ya *National Debt Management Committee (NDMC)* na kubaini mapungufu kadhaa katika maombi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mapungufu hayo yalikuwa ni kukosekana kwa andiko la mradi, uchambuzi yakinifu, kiasi halisi cha mkopo na masharti yake na namna mkopo huo utakavyolipwa. Mawasilisho ya awali ya jedwali la mwenendo wa fedha (*cash flows*) halikuwa na mchanganuo wa kubainisha urejeshaji wa mkopo huo na namna fedha hizo zitakavyotumika. Aidha, tulikubaliana namna bora ya kuandaa jedwali hilo likiwa na maelezo ya ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja juu ya mmiliki wa chuo kikuu ambapo baada ya majadiliano ya kina tulipewa maelezo na Bodi ya Chuo kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ndio mmiliki wa chuo kwa asilimia 100. Aidha, utata mwingine ulikuwa jina la mkopaji ambapo awali ilisomeka kama *Jandu Plumbers* ambayo ni kampuni binafsi inayojishughulisha na ujenzi na uuzaji wa vifaa vya ujenzi ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, baada ya kufanya marekebisho ya kasoro zilizokuwa zimeanishwa na Kamati imewasilisha tena maombi hayo Wizara ya Fedha. Kamati hizo zilipitia maombi hayo tena na kujiridhisha na kisha kuishauri Serikali kutoa dhamana kwa ajili ya mradi huo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ambayo ndiyo yenye mamlaka kisheria ya kutoa dhamana kwa Taasisi/Mamlaka ambazo ziko chini ya TAMISEMI. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 (*Local Government Finance Act*). Kwa hiyo tunashauri Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda iendelee na mchakato wa kupata dhamana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa, taratibu zote zilishakamilishwa na Halmashauri ya Wilaya ikiwemo kufuata taratibu zilizoelekezwa na Wizara. Maombi hayo tuliishayapeleka ofisi ya Waziri Mkuu, lakini hadi sasa bado hatujapata majibu ya dhamana hiyo. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuhimiza suala hili liweze kukamilishwa ili kuwasaidia wananchi wa Wilaya hiyo ya Mpanda na wananchi wa Mikoa ya Kigoma na Rukwa ambako hakuna chuo chochote kile cha kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda iliishapata mbia ambaye angeweza kusaidia kuharakisha ujenzi huo wa Chuo cha

Kilimo ambaye anatoka nchini Uingereza kupitia chuo cha *Royal Agriculture University*. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuharakisha mchakato huu ili uweze kuwanufaisha wananchi wa Mikoa hiyo ya Kanda ya Magharibi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kakoso kwa ufuatiliaji wake ili kuhakikisha ukanda huo unapata chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake yote mawili yana-*relate*, kwanza kwa sababu hizo kasoro zimesharekebishwa basi tutashirikiana pamoja na TAMISEMI kuhakikisha kwamba huo mchakato unakamilika na wanapata dhamana kwa haraka zaidi kadri inavyowezekana. Kwa hivyo, *once* tukiishapata dhamana basi hizo taratibu nyingine za mbia nazo zitakuwa *worked out* kama kawaida. Nipende kumhakikishia Mheshimiwa Kakoso kwamba, maadam hizo kasoro zimesharekebishwa basi Wizara ya Fedha tutashirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba ukanda huo unapata chuo kikuu kwa haraka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la mwisho kwa siku ya leo linaenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na linaulizwa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 395

**Ugonjwa Unaoitwa Gesi**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Watu wengi wanaugua ugonjwa unaoitwa ‘gesi’

(a) Je, nini chanzo cha ugonjwa huo?

(b) Je, tiba ya ugonjwa huo ni nini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge naomba kutoa maelezo yanayohusu tatizo la gesi yafuatayo:-

Kwa kawaida kila mtu ana gesi au hewa tumboni. Gesi hii ni mchanganyiko wa hewa za aina kadhaa kama Oksijeni, Hewa ya Mkaa, Haidrojeni, Methane na *Carbon Monoxide*. Gesi inapokuwa nyingi kupita kiasi, mtu ndipo hulalamika kuwa ana ugonjwa wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali kama kama ifuatavyo.

(a) Gesi inatokana na mambo yafuatayo:-

(i) Mtu kumeza hewa wakati anakula, kunywa au kumeza hewa yenyewe kwa kunywa maji kwa haraka, kunywa vinywaji vyenye gesi nyingi kama soda, kutafuna *chewing gum 'Big G'* kwa muda mrefu na kuvuta sigara.

(ii) Kutengenezwa kwa gesi tumboni kutokana na mmeng'enyo wa chakula katika utumbo mkubwa kilichobaki kutoka utumbo mdogo kunakofanywa na vijidudu ambavyo maskani yao ya asili ni katika utumbo mkubwa.

(iii) Kula kiasi kikubwa vyakula vinavyotengenezwa gesi kwa wingi kama maharage, vitunguu, bia, mvinyo, viazi na vyakula vingine vya wanga, isipokuwa wali.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, tiba ya ugonjwa wa gesi ni kuacha kutafuna *chewing gum 'Big G',* kuvuta sigara, kunywa vinywaji kwa haraka, kupunguza matumizi ya vinywaji vyenye gesi kama soda na bia, kupunguza ulaji wa vyakula

vinavyosababisha uzalishaji wa gesi kwa wingi tumboni na kupunguza kiasi cha chakula kinacholiwa. Ulaji wa chakula kupita kiasi au kuvimbiwa, kunasababisha tatizo la kuwa na gesi nyingi tumboni kwa vile chakula ambacho hakijameng'enywa na kufika kwenye utumbo mkubwa kitakuwa kingi. Aidha, gesi huweza kupunguzwa kwa kunywa mtindi hai, vinywaji vyenye tindikali *(acid)* kama vile juisi ya ndimu au siki.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na kuwapa pole wale wote wanaovuta sigara na kutafuna *chewing gum*, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, ugonjwa huu wa gesi una uhusiano wowote na vidonda vya tumbo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna baadhi ya vyombo vya habari vinatangaza dawa inayoitwa Nitrojeni kuwa inatibu vidonda vya tumbo. Je, Serikali inauambia nini umma kuhusiana na dawa hii? Ahsante.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya wagonjwa wenye vidonda vya tumbo hulalamika kupata hisia ya kuwa na gesi nyingi tumboni. Kwa hivyo, ni vyema wafanyiwe uchunguzi na wapate tiba ya vidonda vya tumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la hiyo dawa anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge, ambacho ninaweza kusema katika suala hili ni kwamba, hakuna dawa inayoruhusiwa kutumika bila ya kuwa imethibitishwa ubora wake kwa kupata kibali maalum kutoka Taasisi ya Chakula na Dawa Tanzania *(TFDA).* Kwa hivyo, ni vyema wanaotumia dawa hiyo wakajiridhisha kwamba imepata hati ya kutoka *TFDA* vinginevyo basi wasitumie dawa hiyo. Nachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, nitafuatilia ili nione kama dawa hiyo ina ubora unaostahili. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MUHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kumezuka watu ambao wana kitu kinachoitwa kama *mobile clinic* wanapita mitaani wakisema wanatibu gesi, presha, sukari na wanaondoa sumu mwilini. Kwa kuwa dawa hizo wanazouza zinaleta athari na kuna watu wameishapata matatizo kutokana na dawa hizo. Je, Serikali ina taarifa hiyo na inatoa tamko gani kama inajua kwamba wako watu wa namna hiyo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chombo maalum cha kutoa vibali kwa ajili ya watu wanaotoa huduma za afya, iwe ni zile hospitali binafsi ambazo ni majengo au viwe vyombo kama hivi vinavyoitwa *mobile clinics* zinazotembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Chombo hicho kinaitwa Bodi ya Usajili wa Hospitali Binafsi na ni lazima mtu yeyote anayefanya shughuli hiyo awe amepata usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kusajili ni kujihakikishia sisi kama wasimamizi wa sekta ya afya kwamba, kwanza ile sehemu ya kutolea huduma inakidhi matwakwa. Pili, wana wataalam wanaostahili kufanya kazi hiyo na kadhalika. Kwa maana hiyo ni kwamba, kama kuna *mobile clinics* ambazo hazina usajili wanafanya hivyo kinyume na taratibu. Tunaomba tupate taarifa hizo na tutachukua hatua stahili.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hivi karibuni kumekuwa na ugonjwa ambao umekuwa ukishambulia watu wengi, ugonjwa wa mfuko wa nyongo kujaa mawe '*gallstones*'. Hata hivyo, ugonjwa huu umekuwa ukifananishwa sana na vidonda vya tumbo na hivyo wagonjwa hao kupewa dawa za vidonda vya tumbo, hali inayosababishwa na hospitali zetu za Wilaya na Zahanati kutokuwa na vifaa vya kubaini ugonjwa huo. Naomba nifahamu Serikali imejipanga vipi kuwasaidia hawa wagonjwa ambao wanaugua *gallstones* na badala yake wanapewa dawa za vidonda vya tumbo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ni kweli kuna ugonjwa wa mawe katika *gallbladder* ambao unaitwa *Cholelithiasis* na mara nyingi unaweza ukachanganywa na vidonda vya tumbo kwa sababu dalili yake kubwa ni maumivu ya tumbo. Ili kubaini kwamba, *gallstones* ndiyo ziko pale, ni lazima itumike *ultra sound* ambapo yale mawe huwa yanaonekana kupitia mashine hiyo na mtu anapata tiba inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kushauri tu ni kwamba kwa vile vituo ambavyo havina mashine hizo za *ultra sound*, basi ndiyo maana kuna utaratibu wa rufaa kwamba, mgonjwa atoke katika kituo kile aende hospitali ya juu zaidi hususan zile za wilaya, aweze kupata kipimo hiki ili tatizo lake liweze kubainika kwa uhakika kabla hajapewa dawa ambazo pengine zinaweza kumdhuru badala ya kumsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kusema hapa ni kwamba, Serikali itaendelea kuhakikisha hizi *ultra sound*, zinafikishwa katika maeneo ya hospitali za Wilaya na pengine chini zaidi. Hivi sasa tuna mradi maalum wa *ORION* ambao unakuja na utaleta zana mpya katika vituo vyote vya kutolea huduma kuanzia ngazi ya Wilaya. Kwa maana hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba, ugunduzi wa magonjwa unafanywa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa ili wagonjwa wasipatiwe dawa ambazo zinaweza kuwadhuru.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Kapt. John Komba, nimewaona na nitawapa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni zetu na taratibu, tumepokea taarifa ya Mheshimiwa Moses Machali, akitaka kuleta Maelezo Binafsi ndani ya Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni zinazostahiki, naomba sasa nimpe nafasi ili aweze kuwasilisha kile alichokuwa anataka kukiwasilisha ndani ya Bunge. Mheshimiwa Moses Machali, unaweza kuendelea, una dakika 15 kwa mujibu Kanuni. Waheshimiwa Wabunge wengi mnafikiri Maelezo Binafsi ni dakika 30, ni dakika 15 tu.

## Maelezo Binafsi ya Mheshimiwa Moses J. Machali juu ya Matumizi sambamba kati ya teknolojia ya Dijitali pamoja na Analojia

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili kusudi niweze kuwasilisha Maelezo Binafsi juu ya matumizi sambamba kati ya teknolojia ya dijitali pamoja na analojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa agizo la Shirika la Kimataifa la Mawasiliano -ITU, mwisho wa urushaji wa matangazo kwa njia ya analojia ni tarehe 17 Juni, 2015 na kwa Afrika Mashariki, mwisho ulitakiwa kuwa tarehe 31 Desemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya teknolojia ya dijitali ni uamuzi wa dunia nzima, hivyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina uchaguzi katika suala hili. Matumizi ya teknolojia hii katika nchi yetu ni muhimu na ni kwa faida ya Taifa letu, kuwa pamoja na jumuiya ya kimataifa katika teknolojia ya mawasiliano. Mbali na Tanzania hakuna nchi nyingine iliyokwishakufanya hivyo. Kwa Tanzania maelezo ya Serikali kupitia *TCRA* yalikuwa kwamba, itazima mitambo ya analojia kuanzia tarehe 1 Januari, 2013 ikianza na Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi sasa mitambo hiyo ya analojia imeishazimwa katika Mikoa mitano na uzimwaji wa mitambo ya analojia ni endelevu kwa Mikoa yote ya Tanzania iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa wananchi wote waliokuwa wanapata matangazo ya luninga kwa njia ya analojia wanapata sambamba kwa njia ya digitali yaani (*voverage area is the same for analogy and digital).*

(i) Mwananchi anachohitaji ni kupata habari, kuburudika na kuelimika kutokana na matangazo ya luninga;

(ii) Ili kupata matangazo hayo anahitaji kisimbuzi yaani *decorder*.

(iii) Visimbuzi vipo vya aina mbili *DVVT* na *DVVT II*. Kisimbuzi cha *DVVT II* kinaweza kupokea matangazo kutoka kwenye mitambo ya *DVVTII* na *DVVT, free to air channels*. Pili, kisimbuzi cha *DVVT* kinaweza kupokea matangazo kutoka kwenye mitambo ya *DVVT* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi baada ya uzimwaji wa mitambo ya analojia hapa nchini. Tatizo la kuhamia katika teknolojia ya digitali ni kubwa kwa wamiliki wa vituo vya luninga na kwa wananchi wa kawaida. Matumizi ya kuhamia kwenye teknolojia hii yamefanywa kwa haraka sana. Kuna wananchi waliokuwa wanapata matangazo kwa njia ya luninga kabla ya kuzimwa kwa mitambo ya analojia ambao sasa hivi hawayapati matangazo hayo baada ya kuzimwa kwa mitambo ya analojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo hapa kwetu kama vile katika nchi nyingi duniani, uamuzi huu umeleta changamoto nyingi. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kukosa uwezo wa kununua kisimbuzi yaani *decorder*; na

(ii) Kutopata matangazo ya digitali kutokana na eneo lao kutofikiwa na matangazo ya digitali wakati enzi za analojia walikuwa wakipata matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata bila ya kufanya utafiti kwa kulinganisha tu idadi ya mitambo ya anolojia iliyokuwepo na ya digitali iliyopo ukweli huu unajidhihirisha. Kwa mfano, Dodoma kulikuwa na mitambo sita ya analojia ambayo ilikuwa ni *ITV, EATV, TBC*, *Star TV, Channel Ten* na *Agape TV*, sasa hivi kuna mitambo miwili tu ya digitali yaani *Star Media* na *Agape Associates.* Mwanza kulikuwa na mitambo sita ya analojia ambayo ni *ITV, EATV, TBC*, *Star TV*, *Channel Ten* na *Agape TV,* sasa hivi kuna mitambo ya digitali yaani *Star Media* na *Agape Associate*. Arusha kulikuwa na mitambo sita ya analojia, *ITV, EATV, TBC, Star TV, Channel Ten* na *Agape TV,* sasa hivi kuna mitambo miwili *Star Media* na *Agape*

*Associates*. Tanga kulikuwa na mitambo mitatu ya analojia *TBC*, *Channel Ten* na Halmashauri ya Jiji la Tanga, sasa hivi kuna mitambo miwili ya *Star Media* na *Agape Associates*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi kulikuwa na mitambo minne ya analojia *ITV, EATV, Agape TV* na *Star TV* kutoka mtambo wa Arusha. Sasa hivi kuna mtambo mmoja wa *Star Media* peke yake. Mbeya kulikuwa na mitambo mitatu ya analojia *TBC, Agape TV* na *Star TV*, sasa hivi kuna mitambo miwili ya digitali *Star Media* na *Agape Associate.* Hata Dar es Salaam ambako kulikuwa na mitambo mingi ya analojia kwa sasa hivi kuna mitambo mitatu ya digitali *Star Media, Agape Associates* na *Basic Transmissions Limited* ambayo imefungwa sehemu mbalimbali za Jiji ambazo ni Kisarawe, Mbezi na Mikocheni bado kuna maeneo ambayo matangazo ya digitali hayafiki. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba hivi karibuni *Star Media* wamefunga mtambo wao katika eneo la Makongo Juu ili kuongeza eneo ambalo matangazo yao yanapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba kuna wananchi wengi hawapati matangazo ya luninga kwa njia ya digitali kutokana na eneo ambalo matangazo hayo kuwa madogo ukilinganisha na wakati wa analojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kuwarahisishia wananchi kupata habari kwa njia ya luninga kwa kuruhusu matumizi ya analojia sambamba na teknolojia ya digitali hadi hapo tutakapokuwa tayari kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kwamba nchi za wenzetu ambako kuna maendeleo makubwa ya teknolojia na uchumi ulio imara zaidi kuliko wetu iliwachukua kati ya miaka sita hadi kumi na nne kurusha matangazo ya luninga kwa njia zote mbili za analojia na digitali kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la hekima na busara kwa Serikali kuruhusu urushwaji wa matangazo kwa

njia zote mbili wakati tukijiimarisha kiteknolojia na kiuchumi kuhakikisha wananchi wana uwezo wa kununua visimbuzi au ving'amuzi au wanawezeshwa kwa Serikali kutoa ruzuku kwa manunuzi ya ving'amuzi ambapo kila mwananchi anaweza kumudu bei ya kununua ving'amuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzimwaji wa mitambo ya analojia hauathiri wananchi peke yao bali pia umekuwa na athari kwa wamiliki wa vituo vya luninga na watayarishaji wa matangazo kwani wenye matangazo ya biashara hasa Makampuni ya Simu ambao ndio watangazaji wakubwa wamesitisha mikataba kutokana na madai kwamba watazamaji wamepungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kutazamwa kwa umakini mkubwa ni utaratibu wa kuhakikisha kwamba matangazo ya vituo vya luninga zote tano Kitaifa yanapatikana katika visimbuzi vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike au napendekeza nini kifanyike. Hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa na Serikali ili kuweza kukabiliana na changamoto za kuhamia katika teknolojia ya digitali.

(i) Kuruhusu matumizi ya teknolojia ya analojia sambamba na teknolojia ya digitali hadi hapo tutakapokuwa tayari kuendana na mabadiliko haya ya kiteknolojia. (*Makofi*)

(ii) Utaratibu wa kuzima mitambo ya analojia kwa Mikoa mingine usitishwe hadi hapo vituo vya luninga vitakapokuwa na uwezo wa kurusha matangazo yao moja kwa moja kwa kutumia teknolojia ya digitali. (*Makofi)*

(iii) Serikali izingatie hali ya kipato cha Mtanzania bila kujali matakwa ya kiteknolojia au ya kibiashara, utu wa Mtanzania ni vyema ukatazamwa kwa jicho la utaifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Machali kwa kujali muda na naona sasa tunaanza kuwa na uzoefu mkubwa wa Kikanuni, kwa kweli umezingatia matakwa yote ya Kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa kiji-*note* kwamba Wabunge mlikuwa hamjapata hiyo nakala ya kile anachokisema Mheshimiwa Machali, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu na ukienda kwenye Kanuni ya 28(8) maelezo hayo yakishawasilishwa kwenye Meza ya Spika, Mbunge anaweza kupewa nafasi kwa idhini ya Spika kuyaleta ndani ya Bunge lakini haizuii Ofisi ya Katibu wa Bunge kuendelea kugawa maelezo hayo kwa Wabunge wengine. Kwa hiyo, kama imechelewa basi nadhani mtapata tu nakala baada ya muda si mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni hizo hizo kuna watu tayari walishaniandikia hapa wanaomba kuchangia hoja ya Mheshimiwa Machali na maelezo aliyoyatoa. Kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2) ambayo inatupa maelekezo, Mbunge anayekusudia kutoa Maelezo Minafsi atapaswa kuwasilisha maelezo hayo mapema kwa Spika na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi 15 na maelezo hayo hayatakuwa na mjadala kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo wale waliokuwa wamejianda kwa nguvu sana kuchangia jambo hili, Kanuni inanikataza kabisa na hawana nafasi ya kulichangia. Badala yake basi tunaiomba Serikali ipokee hayo Maelezo Binafsi na tunaamini kabisa kupitia tena Kanuni zetu na nadhani ni Kanuni 41 kama sikosei basi Serikali mtakuja na Kauli ndani ya Bunge ili kutoa maelezo kuhusiana na hiki ambacho Mheshimiwa Machali amekisema na Watanzania wote waweze kuelewa hilo linaloendelea na Serikali mmefanya nini na mmejipanga vipi katika mfumo huu wa uhamaji kutoka analojia kwenda kwenye digitali.

Waheshimiwa Wabunge, lakini Waswahili wanasema ni '*digit*' Mheshimiwa Machali sio digitali ni *digit*, kisimbuzi, *digit*. Kwa hiyo, tumehama kutoka kwenye yale maneno mengine yote sasa hivi tunasema ni *digit*. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge huo mfumo wa *digit* utapewa maelezo humu ndani ya Bunge kupitia kauli ya Serikali.

Nilikuona Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Kessy na Mheshimiwa Kapteni Komba, kwa hiyo niwape ruhusa ya Miongozo kabla sijatoa matangazo yangu. Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) nikiomba Mwongozo wako, lakini nikirejea kanuni ile ya 64(1) (a) na (g).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 inasema hivi:-

"*Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-*

*(a) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli; na ile ya*

*(g) Hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Leticia Nyerere, alipouliza swali Namba 390 kwa niaba ya Mheshimiwa Olupulukwa alisema kwamba "Askari wetu wanavaa nguo ambazo zimejaa viraka kila pahali". Sasa kauli hii kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni ya kudhalilisha Askari wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida labda Kiti kituongoze kama kweli Mbunge anaweza akathibitisha kwamba Askari wetu ambao wengi tunakutana nao barabarani na tunawaona na wengine tunao hapa Bungeni kama kweli *uniform* wanazovaa zimejaa viraka kila pahali. Nakubali inawezekana ziko changamoto lakini kwamba wanavaa nguo ambazo zimejaa viraka kila pahali, huku ndiko kuwadhalilisha Askari kinyume na yeye kusema kwamba Askari hawa wanadhalilishwa na Serikali. Sasa ninaomba utoe *ruling* yako, ni sahihi kwa Mbunge kusema taarifa za namna hiyo Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme kwamba leo ni siku ya kuzaliwa kwangu, natimiza miaka 51, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, ahsante sana. (*Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kumbe bado mdogo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kessy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako, Kanuni 68(7) kutokana na swali Na. 395 kuhusu gesi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kessy umesema unatumia Kanuni gani?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kanuni ya 68(7).

**MWENYEKITI:** Ahaaah!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Swali la 395 kuhusu gesi. Naomba lifafanuliwe vizuri maana yake wananchi wanaweza kufikiri ile gesi ambayo iko matumboni mwao ni sawa na ile gesi ya Mtwara wakaanza kutafuta wawekezaji? (*Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako isije ikawa matatizo. Maana yuko mama mmoja wa Mtwara aliambiwa ana gesi akasema anatafuta mwekezaji yeye mwenyewe, hii inaweza kuwa hatari. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hii kazi kweli kweli. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 46 inayosema…

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi Mheshimiwa Kapteni?

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Kanuni ya 46.

**MWENYEKITI:** Taratibu kidogo.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA**: Ambayo inasema:-

"Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama ilivyoulizwa..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu nilikuwa nimeuliza swali la nyongeza linalohusu mazingira, swali la msingi lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Thuwayba Idrissa Muhamed. Niliuliza habari ya samaki kufa kule Ziwa Nyasa halafu wanaelea majini na wanakuja nchi kavu halafu wananchi wanaokota wanakula. Kwa hiyo, kuna wasiwasi pengine samaki wale ambao wana sumu au wana kitu kingine ambacho hakijaeleweka. Nilitaka Serikali ichukue nafasi ya kupeleka wataalamu wake kule lakini jibu la Waziri halikunifurahisha hata kidogo, ananituma mimi niende nikaonane na Afisa wake huko chini, sijui Afisa wa Mazingira, sijui Afisa Samaki, hiyo si kazi yangu mimi Mbunge, kazi yangu ni kuibana Serikali hapa iende kule, sio mimi niende huko. Je, kwa jibu hilo, sio Waziri hajanitendea haki na hiyo sio kudharau kazi ya Mbunge na hii sio kudharau wananchi wanaokula samaki bila ya kujua kama wana sumu ama hawana sumu? Naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge wote watatu kwa Miongozo yenu.

Nianze na Mwongozo wa Mheshimiwa Keissy, huu Mwongozo kwa kweli ni mgumu sana na majibu yake kwa kweli ni mazito sana. Sasa kama hata Mheshimiwa Keissy hajaelewa hii gesi iliyozungumzwa hapa na anataka ufafanuzi utolewe basi mimi ngoja tu niwaambie Watanzania kwa sababu Keissy ameomba, gesi iliyokuwa inazungumzwa ni tatizo la ugonjwa ambao uko ndani ya tumbo la binadamu, lakini si gesi ile inayochimbwa ardhini ambayo Mheshimiwa Keissy anaizungumzia hapa na hususan gesi ambayo iko huko Mtwara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy nafikiri Watanzania watakuwa wamenielewa na hata wewe kama ulikuwa una wasiwasi hujaelewa vizuri na labda ulikuwa na tatizo la gesi

ukafikiri gesi ya Mtwara imehamia tumboni mwako basi naomba tu uwe na amani gesi ya Mtwara huwa haihamii kwenye matumbo ya binadamu.Kama bado una wasiwasi Mheshimiwa Keissy unaweza kukutana na Madaktari wetu hapo wakakupima ili kujua kama una gesi ya Mtwara ama una gesi ya tumbo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea Mwongozo wa Mheshimiwa Zambi. Mheshimiwa Zambi ametumia vifungu viwili, kwanza ametumia Kanuni inayomruhusu Mbunge kuomba Mwongozo, lakini akarejea kwenye Kanuni ya 64(a) na (g). Sasa Mheshimiwa Zambi kwa Kanuni hii ya 64(a) hiyo siwezi kukupa Mwongozo kwa sababu na wewe mwenyewe umekiuka Kanuni. Unapomtuhumu Mbunge amesema uongo ni lazima wewe mwenyewe kwanza utoe maelezo na kuthibitisha ule uongo aliousema Mbunge kwa kuleta maelezo ya kimsingi ambayo ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika lile la (g) la udhalilishaji, hoja yako pale ndiyo ingeweza kuwa na msingi mkubwa. Kwa matamshi yale kwa kweli kwa wale Askari wetu huwezi kujua huko nje wamejisikia namna gani kwa matamshi ya namna hiyo. Sasa ili kuliweka hili wazi na bayana na kueleza picha ya Serikali katika kuwahudumia Askari wetu, mimi ningewaomba Serikali mngekuja hapa Bungeni na Kauli ya Waziri aeleze kwa ufasaha hali ya Askari wetu walivyo ili kuweza kuwapa picha Watanzania juu ya haya yaliyosemwa kwamba wametembea nguo zao, ni kitu ambacho kwa kweli kinaweza kuwa hakijabeba sura nzuri sana. Kwa hiyo, nitawaomba sana Serikali mje kuwaeleza Watanzania kama hivyo sivyo hali ilivyo, itapendeza sana kama Serikali mtasema ili Watanzania waweze kuelewa, kwa hiyo, hili nalirudisha kwenye mikono ya Serikali.

Nikija kwenye Mwongozo wa Mheshimiwa Kapteni Komba, kwanza niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri, kunapotokea matatizo makubwa ambayo yanaweza kuwa yana athari kubwa kwa wananchi, nafikiri kuna umuhimu wa kukubaliana na Wabunge kufanya tafiti za kuweza kuwasaidia wananchi mahali walipo. *(Makofi)*

Ni kweli Mheshimiwa Mbunge na wewe una wajibu wa kufanya kazi hizo kwa niaba ya wananchi, lakini Mbunge atakapoleta suala hapa ndani, inawezekana liko tatizo kubwa la kimsingi. Kwa hiyo, ningemwomba sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Huvisa pamoja na kumwagiza Kapteni Komba kwenda kulifuatilia suala hilo, ninakuomba wewe kwa niaba ya Serikali kufanya utafiti na kujua ukweli wa tatizo hilo. Kama kweli samaki wanakufa kwenye Ziwa Nyasa na wananchi wa Mwambao wa Ziwa Nyasa wanawala samaki hao halafu nguvu hiyo tukaiacha kwa Mbunge peke yake, tunaweza kuhatarisha afya za Watanzania bila ya kuwa na sababu ya msingi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningekuomba sana Mheshimiwa Waziri ushirikiane na Mheshimiwa Mbunge aliyetoa taarifa hii mpate ukweli wa jambo hilo na lishughulikiwe mapema na kujua ukweli wake na kuokoa maisha ya Watanzania ambao labda huyu Kapteni Komba akichukua hatua zinaweza kutumia muda mrefu na zisifikie mwisho kwa haraka.

Kwa hiyo, ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri tushirikiane katika kutatua matatizo ya Watanzania na wakati mwingine, Waheshimiwa Mawaziri naomba m-*draw attention* katika maelezo ninayoyatoa. Waheshimiwa Mawaziri, ningeomba sana mnisikilize, ninatoa maagizo, Mheshimiwa Dkt. Huvisa, ninatoa maagizo, ningeomba sana mheshimu Kiti msikilize ninachokisema ili muweze kwenda kutekeleza vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ndani ya ukumbi wa Bunge. Kwanza, kuna viongozi wa Sekretarieti za *APNAC* kutoka katika nchi kadhaa za Bara za Afrika na wamekaa kwenye jukwaa la Spika pale nitawambulisha kwa majina yao na nitawaomba wasimame ili waweze kufahamika kwa Wabunge wetu. Wageni hawa ni hao wafuatao:-

Mheshimiwa Cornelius Mweetwa, Mwenyekiti wa *APNAC* Zambia, karibu sana. Mheshimiwa Lucky Mulusa, Mjumbe wa Kamati Tendaji ya *APNAC* Zambia. Mheshimiwa

Mbiji Mufalo, Mshauri wa *APNAC* kutoka Zambia, karibu sana. Tuna Ndugu Daniel Batidam, Mkurugenzi Mtendaji wa *APNAC* kutoka Sekretariet ya *APNAC* iliyopo Accra, Ghana ameambatana na Watendaji watatu kutoka Accra, Ghana. Ahsante, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wageni wetu hawa mwenyeji wao waliyeambatana naye ni Prof. David Mwamfupe ambaye ni *Dean* wa *Faculty* ya *Social Science,* Chuo Kikuu cha Dodoma na ni Mshauri wa *APNAC* Tanzania. Profesa nafikiri hayupo. (*Makofi)*

Tunao wageni wengine waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, kwanza kabisa, wako wageni waliomsindikiza Mheshimiwa Aeshi Hilary baada ya kushinda kesi ya uchaguzi, watu wa Sumbawanga kwa kuonyesha umoja na mshikamano, wamemsindikiza Mbunge wao na hao ni pamoja na wafuatao:-

Kundi la kwanza, ni Kamati ya Siasa ya Mkoa ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa. Kamati ya Siasa ya Wilaya ikiongozwa na Katibu wa Siasa wa Wilaya, naona wamekaa huko juu. Madiwani wa Sumbawanga Mjini wakiwemo Madiwani wafuatao kutoka Upinzani, Mheshimiwa Fides Kasitu, Diwani wa CHADEMA, Mheshimiwa Mavazi, Diwani wa DP, Mheshimiwa Laureana Mavazi, DP, Mheshimiwa Nestory Msengezi, Diwani wa CHADEMA, Mheshimiwa Amina Muhako, Diwani wa CHADEMA, aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA Wilaya, Ndugu Hashim Komba na Ndugu Daniel Maginga. Kwa hiyo, hao wameambatana pamoja na Madiwani wengine.

**WABUNGE FULANI:** Wako wapi?

**WABUNGE FULANI:** Wa CHADEMA hatujawaona.

**MWENYEKITI:** Wapo nadhani huko juu.

**WABUNGE FULANI:** Wapi?

**MWENYEKITI:** Kwa sababu tayari majina yao ninayo hapa, ina maana wapo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na matangazo yetu, tunao wanafunzi 62 na Walimu wao kutoka Shule ya *Hill Crest Junior Academy* ya Sumbawanga, ni Waheshimiwa wa mtaalamu wa gesi, Mheshimiwa Keissy. *(Kicheko)*

Tunao wanafunzi 50 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Mikocheni Dar es Salaam. Nafikiri hawa wageni watakuwa *basement,* nadhani wengi hawajaingia hapa ndani.

Tunao wanafunzi 35 na walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Kilombo. Tunao wanafunzi 108 kutoka Chuo cha Ufundi VETA, Dodoma na tuna wanafunzi 52 na Walimu nne kutoka *Southern Highland School,* nafikiri na wao wameshatoka.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo hapa tangazo na kweli ninafikiri nilitangaze hili. Kwanza, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge Wanawake na hasa wale Waheshimiwa Wabunge Wanawake ambao pamoja na kazi zao za Ubunge lakini wameweza kutekeleza na majukumu ya uzazi wakiwa ndani ya Bunge. Sasa kwa heshima yote kwa kweli naomba nimtambulishe mtoto Nico, mtoto wa Mheshimiwa Esther Matiko, yuko hapa ndani leo kuangalia shughuli za Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Hebu mnyanyueni huyo mtoto aliyekuja kutushuhudia na leo ni *birthday* yake. Sasa kuna Wabunge hapa wananiuliza baba yake yuko wapi, hiyo namwachia Mheshimiwa Esther mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine, Mama Kippa ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma, Skuli ya Sanaa na Lugha, wana maonyesho ya kazi za sanaa zinazofanywa na wanafunzi wanaosoma Shahada

ya Sanaa na Ubunifu. Maonyesho hayo ni muhimu kwa chuo chetu na wanafunzi hao katika jitihada za kukitangaza chuo na pia Idara inayohusika, wanafanya maonyesho katika eneo la viwanja vya Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kuona maonyesho hayo na wale watakaoweza kununua, waweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba leo tarehe 12 Juni, 2013, mara baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi 227.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine hapa, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kuwa leo Shughuli za Bunge zitaahirishwa mapema, anaiomba sana Timu ya Bunge washiriki kwenye mazoezi jioni saa 10.00 kwa maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Benki ya *NMB*, mchezo huo utafanyika siku ya Jumamosi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Azzan anawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wanamichezo, jioni ya leo kuna umuhimu sana wa kuhudhuria mazoezi na zile Kamati za Ufundi nafikiri zingeanza mapema na kama kawaida Mama Hewa umepotea sana tunaomba leo uwepo uwanjani, Kamati za Ufundi zianze kazi mapema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine pia kutoka kwa Mama Kippa, ananiomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tarehe 15 Juni, 2013 itakuwa ni Siku ya Jumamosi kutakuwa na tafrija ya kumpongeza Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mbunge kwa kulitumikia Bunge hili kama Spika kwa kipindi cha mwaka 2000 - 2005. (*Makofi*)

Tafrija hiyo itafanyika katika viwanja vya Bunge eneo la Maegesho ya Magari ya Wabunge kuanzia saa 1.30 jioni. Tukio hili ni la muhimu kwa Bunge letu hivyo Wabunge wote mnatakiwa kuhudhuria. Tunaomba siku ya Ijumaa,

Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize hapa, magari yasiegeshwe kwenye eneo hilo kwa sababu maandalizi kabambe yatakuwa yameanza na Wabunge wote wanaalikwa kufanya mazoezi kwa ajili ya muziki utakaoporomoshwa siku hiyo na bendi mbalimbali ambazo zimeandaliwa, sasa mazoezi yatafanyikia wapi hiyo ndio sielewi. (*Makofi*)

Kwa mujibu wa Kanuni, naomba tangazo hili ni-*declare interest* ni la kwangu mwenyewe, lakini naomba tu kuwashirikisha, kwa wale watakaopata nafasi leo, ghorofa ya pili, ukumbi wa Pius Msekwa, nitakuwa na ibada ya kumbukumbu ya miaka mitatu ya kifo cha mume wangu. Kwa wenye nafasi, naomba mje tushirikiane pamoja. Kutakuwa na ibada pale na Waheshimiwa Wabunge kadhaa wameshaanza kunisaidia kufanya maandalizi.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, nimeombwa na Katibu wa Bunge niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo siku ya Jumatano tarehe 12 Juni, 2013 kutakuwa na semina inayohusu shughuli za *MSD* kuanzia saa 5.00 katika ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, baada ya hapa wote tunahamia Pius Msekwa kwenda kushirikiana kwa pamoja kwenye semina inayohusu masuala ya *MSD*.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa shughuli za leo, baada ya shughuli hizi kukamilika, ninawaomba sasa niahirishe shughuli hizi za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu.

*(Saa 4.47 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 13 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*